

**MAFUNZO KWA WANACHAMA WA
CHAMA CHA AKIBA NA MIKOPO CHA
WALIMU MOSHI VIJIJINI (MRT
SACCOS LTD) -KILIMANJARO**

CYRIL KALEMBANA KOMBA (PHD)

BEATRICE JUDICA KIMARO

CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MOCU)




**MAISHA KABLA NA BAADA YA
KUSTAAFU**

❖ **SACCOS: HULETA WATU MAKINI
KWA PAMOJA**

❖ **SACCOS: SULUHISHO LA MTAJI**

❖ **SACCOS: FAMILIA YENYE
FURAHA**



- Kustaafu ni msimu mpya ni kipindi ambacho mambo mengi hubadilika kwa sababu kustaafu utumishi ni kubadilisha mfumo wa maisha kutoka katika *ajira na kuanza maisha ya kufanya kazi na jamii.*
- **Kustaafu** ni kuacha kazi kwa mujibu wa sheria, ama baada ya mkataba wako kuisha au kwa kuomba kutokana na sababu mbali mbali kama za kiafya n.k na unapata haki zako. (*yaani huna kazi tena labda kwa mkataba mwengine*). 

- Mbali na mabadiliko hayo, hiki ndicho kipindi unapaswa kuishi maisha ya utulivu zaidi kuliko ilivyokuwa awali...*unapaswa kula vyakula bora ili kuimarisha afya yako*
- Kumeshuhudiwa watu wengi wakiishi maisha ya taabu na karaha na mahangaiko makubwa baada ya kustaafu ,hili linatokana na kutojiandaa vyema kabla ya kustaafu.
- Na suala la maandalizi ya kustaafu yanatakiwa kuanza mara tu baada ya unapoajiriwa.

!!...USTAAFU NI TUNU NA HESHIMA...!!

- ✓ Anza maisha ya kustaafu usisubiri kiinua mgongo
- ✓ Maandalizi hayo utayafanya kupitia MRT SACCOS LTD pekee
- ✓ Achana na imani kuwa ukipata kiinua mgongo taabu zako zitakuwa ni historia-unajidanganya



HALI ZA WATUMISHI KABLA NA BAADA YA KUSTAAFU

- ❖ Hufa wakiwa kazini kutokana na kufanya kazi kwenye mazingira yasiyo salama kiafya kama joto au vumbi la viwandani, kuambukizwa magonjwa kwenye mahospitali, ajali kwenye majeshi n.k.,
- ❖ Huishia kuwa tegemezi kwa watoto waliowazaa, ndugu na wengine kuomba misaada,
- ❖ Kuendelea kufanya kazi za mikataba kwa malipo madogo
- ❖ Wachache sana huwa wanauwezo wa kuendesha maisha ya kawaida bila shida NA,
- ❖ Wachache zaidi sana huwa matajiri baada ya kustaafu
(HAWA NI WALE WALIOJIANDAA VIZURI KAMA KUWEKEZA KWENYE SACCOS)



Tunajifunza nini kutokana na hali halisi hiyo?

- Kwa vyovyote vile, hali hizo zinatoa kiashiria kuwa wastaafu wengi wana hali mbaya na tete.
- Tunakumbushwa tuanze kufanya maandilizi mapema, tena mara moja **(WEKEZA KATIKA CHAMA CHAKO CHA MRT)**.
- Vinginevyo utaangukia kwenye kundi la maisha yasiyofaa uzeeni na kibaya zaidi utakuwa huna nguvu kama ulivyo sasa kabla ya kustaafu
- Fursa za uwekezaji ulizonazo sasa ni vema ukazitumia vizuri sasa na baada ya kustaafu **(WEKEZA KATIKA CHAMA CHAKO CHA MRT)**.



MAKOSA MENGI WAFANYAO WATU WENGI BAADA YA KUSTAAFU

- Ujenzia/ununuzi wa nyumba za makazi/magari
- Kufanya miradi wasiyokuwa na uzoefu nayo
- Kudhani kiinua mgongo ni fedha nyingi sana
- Kuamini pensheni ni kubwa
- Kugeuza kiinua mgongo kuwa mali ya ukoo



- Kuwa na wategemezi/watoto wadogo wa uzeeni
- Hawakuwekeza/kutengeneza vyanzo vingine vya mapato
- Kuingia katika ndoa za uzeeni
- Kutumia mafao kama mtaji wa kisiasa



NINI KIFANYIKE KABLA NA BAADA YA KUSTAAFU?

- ❖ Jiandae kisaikolojia
- ❖ Weka akiba na Wekeza kwa maisha ya leo na ya baadae
- ❖ Epuka madeni an Lipa madeni
- ❖ Ondoa matumizi yasiyo ya lazima
(TOFAUTISHA MAHITAJI NA MATAKWA)
- ❖ Tafuta chanzo kingine cha pesa
- ❖ Ongeza na tafuta fursa za kujikinga na majanga baada ya kustaafu
- ❖ Fikiria nje ya boksi
- ❖ Waandae watoto kwa maisha ya kujitegemea


- ❖ Matumizi yako yasizidi mapato yako
- ❖ Panga maisha ambayo ungependa uishi baada ya kustaafu
- ❖ Fanya upendalo na utakalo, kamwe usiige maisha ya wengine
- ❖ Soma vitabu, tembea, talii, pumzika
- ❖ Pata muda wa kuwa na wajukuu, cheka na cheza nao
- ❖ Punguza msongo wa mawazo
- ❖ Samehe na kusahau (kustaafu siyo muda wa kuwaza waliokukosea, waliokudhulumu n.k
- ❖ Andaa malengo yako ya baadae


KUSTAAFU NI TUNU NA HESHIMA



- Shirikisha jamaa wa familia (baba/mama/watoto) katika jambo lolote la maendeleo unalowaza kulifanya kabla na baada ya kustaafu.
- Kuwa na Bajeti yenye uhalisia wa kipato chako
- Kuwa na mfumo wa Udhibiti wa Ndani wa matumizi
- Kufanya Ukaguzi wa mara kwa mara sehemu ya kuhifadhia vyakula na mali za familia
- Punguza/dhibiti matumizi yasiyo ya lazima na ambayo hayapo kwenye bajeti ya familia.

NAMNA YA KUANDAA MALENGO

- ❖ Anagalia hali ya sasa kwenye hilo lengo lako ikoje
 - ❖ Zingatia muda unaotakiwa ili uweze kufikia lengo husika
 - ❖ Tambua nani atakuwa mhusika mkuu wa hilo jambo ili liweze kutekelezeka?
 - ❖ Tambua wahusika wengine
 - ❖ Tambua vitu/mahitaji/rasilimali muhimu katika kufanikisha lengo husika
 - ❖ Andaa bajeti inayohitajika kufanikisha lengo lako (ainisha mahitaji ya kifedha)
- 



NAMNA YA KUFANIKISHA MALENGO

- Watu wengi wamekuwa wakiandaa malengo lakini muda waliojiwekea unapofika hujikuta wakiwa hawajafanikiwa.
- Ili kufanikisha lengo lazima uwe na nia ya dhatai kabisa kutoka moyoni
- Na utakapofanikiwa ni vema ukajipongeza ili kupata hamasa ya kutamani kufikia malengo makubwa zaidi.



Ili uweze kufanikiwa kwenye malengo hakikisha unafanya yafuatayo:-


- Jitambue na ujisimamie mwenyewe**
 - Tambua haupo duniani kwaajili ya kuzurura bali kuacha alama
 - Ukiwa mtumishi wa umma ona aibu kuwa na maisha yasiyoeleweka
 - Aibu hiyo igeuze kuwa fursa aua hamasa



❑ **Fanya jambo kwa wakati sahihi**

- Muda ukipita haurudi nyuma hata kidogo
- Hakikisha unafanya jambo sahihi kwa muda sahihi ili uweze kufanikiwa
- Kuna fursa za msimu hivyo ukiwa mzito kufanya maamuzi ya kuzifikia utakuwa ukichelewa mara kwa mara

❑ **Fanya jambo kwa watu sahihi**

- Hakikisha uwekezaji unafanya eneo sahihi na kwa watu sahihi
 - ❑ **Kuwa na timu sahihi ya utendaji kazi**
 - Ni muhimu kuwa na watu sahihi wakufanya nao jambo husika
 - Ili lengo litimie ni vema lipate mtu sahihi
- 

NAMNA YA KUFIKIA MALENGO

- ✓ Anza kidogokidogo kwa kuweka fedha za dharura na akiba
- ✓ Fanya kitu unachotaka kufanya toka moyoni mwako usiige
- ✓ Kuwa halisi usighushi mambo ili uonekane uko vizuri kumbe sivyo
- ✓ Shirikisha wengine pale inapobidi
- ✓ Jipongeze kila atua unayopiga kufikia lengo lako
- ✓ Panga bajeti ya wiki, mwezi au robo mwaka, nusu mwaka ya mwaka mzima ili kufanikisha malengo
- ✓ Kuna miezi ambayo huwa matumizi yanakuwa makubwa kuliko mingine iwekee alama ili ujipange vizuri
- ✓ Mwiaho wa mwaka fanya tathimini



MADHARA YANAYOWEZA KUTOKEA IWAPO UTASTAAFU BILA KUJIANDAA

- Mstaafu kuwa magonjwa ya msongo wa mawazo.
- Mstaafu kupata athari ya kisaikolojia, hii hufanya mstaafu kukosa raha na heshima mbele ya Jamii inayomzunguka.
- Jamii kukuangalia mzee mstaafu kwa mtazamo tofauti.
- Huleta mfarakano ndani ya familia kwa uhasama kati ya wanafamilia ua na ukoo.
- Hufanya MSTAAFU kutoaminika katika jamii na taasisi za kifedha.

FAIDA ZA KUTASTAAFU KWA KUJIANDAA NA KUWA MWANACHAMA WA CHAMA CHA AKIBA NA MIKOPO

- ❑ Kuwa na uwezo wa kumudu mahitaji ya kila siku kwenye familia
- ❑ Kuwezesha kuendelea kuaminika katika jamii
- ❑ Kuendelea kupata huduma za SACCOS kama mwanachama mstaafu uliyewekeza Chamani
- ❑ Kuimarisha uweza wa kifedha wa mtu binafsi (msaafu)
- ❑ Kuepuka kuwa mtumwa wa shida ndogondongo za kila siku
- ❑ Kutoshawishika kukopa kwa wakopeshaji makanjanja na matapeli AU mikopo kila taasisi ya kukopesha
- ❑ **KUKUZA MTAJI WA CHAMA**



MAISHA YA KUSTAAFU NA UWEKEZAJI UWEKEZAJI KATIKA ASASI ZA FEDHA (MRT SACCOS)

Kuna baadhi ya changamoto za uwekezaji zinaweza kutatuliwa/kuondolewa kabla na baada ya kuwekeza kama vile:

- Epuka uwekezaji usio na tija
- Kuza mtaji kwaajili ya kuwekeza
- Imarisha usimamizi wa uwekezaji husika
- Fanya upembuzi yakinifu (Risk & Return analysis)
- Gawanya fedha zako katika fursa mbalimbali
- Kuwa mbunifu
- Jali afya yako



STAAFU NA MRT SACCOS

Amefanyeje?

**Amestaafu bila
maandalizi**





**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA
MUNGU AWABARIKI**

MWISHO WA WASILISHO

